**Learning by Ear 2011/2012 – Corruption – The Elephant in the Room**

**Episode 04 – "Corruption: The tickle down effect"**

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck, Friederike Müller, Pendo Paul**

**Proofreading: Charlotte Collins, Pendo Paul**

**KISUAHELI: Eric Ponda**

CHARACTERS:

- NARRATOR

Scene 1:

- Fred (MALE, 55)
- Mwichuli (MALE, 50)
- Karanja (MALE, 60)
- John Maina (MALE, 55)
- NARRATOR

Scene 2

- Alfayo (MALE, 58)
- Mwichuli (MALE, 50)
- NARRATOR

Scene 3

- TV Anchor (FEMALE, 40)
- John Maina (MALE, 55)
- Alfayo (MALE, 58)
- Isaac (MALE, 22)
- Sylvia (FEMALE, 19)
- Jennifer (FEMALE, 55)
- NARRATOR

**Intro:**

**0. Narrator:**

Hujambo na karibu kusikiliza sehemu ya nne kwenye mfululizo wa vipindi vya ‘Learning By Ear’ “**Noa Bongo Jenga Maisha yako**” katika mchezo huu wa redio kuhusu suala la ufisadi . Ni hadithi inayosumulia hali halisi ya maisha kwa jina “**Tembo Nyumbani**”

Ama kwa hakika, mambo wanayopitia familia ya Adhiambo ni udhihirisho kamili wa jinsi ufisadi unavyoathiri maisha ya kila mmoja wetu. Lakini upo uwezekano wa kila mtu kuchukua msimamo katika kupambana na uovu huu.

Katika kipindi kilichotangulia, Jennifer anaandamwa na baba ya mmoja wa wanafunzi shuleni, kujaribu kumhonga ili aweze kuimarisha matokeo ya mtoto wake. Jennifer anawasilisha kesi hiyo kwa mwalimu mkuu, lakini anashangaa kuona jinsi gani mwalimu huyo mkuu alivyotawaliwa na ufisadi. Kwa upande mwengine, familia ya Odhiambo inajaribu kumshawishi rafiki yao mkubwa Jeffrey, kuzindua shirika la kibinafsi la kuchunguza visa vya ufisadi. Jeffrey amegundua kashfa kubwa katika sekta ya nishati na anataka kuifichua kabla ya uchaguzi mkuu kuwadia.

Katika kipindi cha leo “UFISADI: Athari zake mashinani” wabunge wanaohusika katika kashfa hii wanakutana kupanga mikakati ya uchaguzi mkuu. Hapana shaka wanahitaji pesa zaidi kufadhili kampeni zao, na njia rahisi na ya mkato ni kupitia ufisadi.

## Scene One:

**1. Atmo:** **Noble Bar atmo, Talking, laughing, drinking**

**2. Fred:** John Maina! Twakutakia kila la kheri rais wetu mtarajiwa! Kwenye vyombo vya habari wametangaza kwamba unawaongoza wagombeaji wengine katika mkumbo huu. Na wewe ndie utakayeiokoa nchi hii - mbali na kutusaidia kujaza mifuko yetu! **(laughs and cheers all round)**

**3. SFX:** **Clinking of glasses**

**4. Mwichuli:** Sssh, Fred, usiongee kwa sauti ya juu. Lazima uwe muangalifu unapozungumza hadharani!

**5. Fred:** Ah wacha wewe , mwichuli,..! hii ni klabu ya wanachama pekee! Na sisi sote ni genge moja kisha kutoka kabila moja! Sote tunaelewa tunachofanya, na mbinu tutakazotumia kuhakikisha tunasonga mbele katika kumsaidia mmoja wetu. Kwani hakuna anayeweza kusaliti watu wake.

**6. Karanja:** Hebu sikilizeni na msikilize kwa makini..! kama wasemavyo, sote tunakula kutoka chungu kimoja! **(more laughing and cheering).** Sawa, tunamsimamisha John Maina, kugombea wadhifa wa urais! Hivyo, hatuna wasi wasi wa siku zijazo na mipango yetu ya baadaye na bila ya kusahau mambo mazuri yanayoandamana na wadhifa huu. Lazima tujitolee kuhakikisha tunafadhili kikamilifu kampeni zake. Lakini pesa hizi zote zitatoka wapi? Mwichuli, wewe si ni mtaalam wa mambo haya?

**7. Mwichuli:** Naam- John tumekuwa tukijadiliana kuhusu suala hili. Hizi pesa tutazipata kutokana na kandarasi zinazotolewa katika sekta ya nishati. Mpango huu umefaulu sana na hakuna mtu hata mmoja ambaye ameshuku kinachoendelea. Hivyo mambo yanakwenda vizuri, kwanini tusiuendeleze? Hapaja haribika jambo na usiwe na wasi wasi – sawa John?

**8. John Maina:** Sawa, Mwichuli. Yaonekana tuna watu wa kutosha katika kambi yetu ambao wako tayari kabisa kuchangia! Na mimi kama waziri wa nishati bila shaka nitaweza kukabiliana na mtu yeyote atakayeleta za kuleta na mizengwe!

**9. Mwichuli:** Kwa mujibu wa mwenyekiti wa halmashauri ya kupambana na ufisadi kile kinyangarika, ‘ mwanachama’ aliyekuwa akileta mdomo amefutwa kazi. Kwa hiyo, nadhani hakuna pingamizi yoyote sasa.

**10. Karanja:** Sawa kabisa .Basi naamini mambo yatakwenda barabara. Kuna yule mfanyabiashara anayeitwa Odhiambo ambaye amekuwa akituuzia vifaa vya huduma za umeme. Kwa hakika lilikuwa jambo la busara kumpa yeye kandarasi hii, kwani kupitia kwake, biashara yetu inaonekana halali. Hakuna mtu anayeishuku! Hata kama hatuzalishi umeme lakini tunazalisha pesa! Haya ndio manufaa ya ujasiriamali wa kutumia akili: tunatengeneza pesa, pasipo kutoa jasho... Hahaha! … **(Laughter)**

**11. Fred:** Ni kweli, Karanja, sioni matatizo.

**12. Mwichuli:** Ili kupata pesa za kutosha kufadhili kampeini za Bw. John Maina, na kisha kusalia na pesa mfukoni, lazima kiwango cha usambazaji umeme kiongezeke! Lakini hilo si tatizo, na

isitoshe wakati John atakapochaguliwa, bila shaka atatuongezea kandarasi hizi.

**13. John Maina:** Kwa hiyo, tufahamu kwamba Ikulu tuko nayo hapa na yenye kutupa matumaini makubwa! **(laughing and cheering)**

**14. SFX** **Clinking of glasses**

**End of scene**

**15. Narrator:** Mambo yanazidi kupamba moto. Wanasiasa na wafanyabiashara hawa, hawana aibu wala kujali maslahi ya watu wanaodai kuwaaakilisha. Muhimu kwao ni kumtapeli kila mmoja ilmradi kuona kwamba wametajirika. Na ufisadi huu unaanzia juu. Mara nyingi hawatendi fadhila eti kutokana na moyo wao wa huruma, bali kwa kutarajia malipo au manufaa fulani, iwe pesa au vinginivyo. Na ndio chanzo cha kukita mizizi kwa ufisadi miongoni mwa jamii.

## Scene Two:

**16. Atmo:** **Minibus driving, loud music**

**17. Alfayo:** **(phone ringing)** Hello? **(shouting above music)** Hallo, hallo, unanisikia?

***KW Begin (without Minibus-Atmo)***

**18. Mwichuli (via phone):** Alfayo Odhiambo? Nahitaji kuzungumza na wewe!

**19. Alfayo:** Hello? Nani huyo? **(louder, to bus driver)** Hebu nishuke, tafadhali unaweza kusimamisha basi? **(to phone)** Hallo, Sikusikia vizuri, subiri nishuke kutoka kwa hili basi, subiri kidogo tu!

**20. SFX:** **Minibus stops, bus door slams shut, Drives off**

***KW End***

**21. Atmo:** **Street noises in the background**

**22. Mwichuli (via phone):** Alfayo. Mimi ni Mwichuli.

**23. Alfayo:** Ohh… sawa. Kuna nini?

**24. Mwichuli (via phone):** Kwa ufupi .Uchaguzi unakaribia na waziri wetu wa nishati John Maina anagombea Urais. Tunahitaji utuuzie shehena kubwa zaidi ya mita za umeme. Unadhani ni lini unaweza kufanya hivyo?

**25. Alfayo:** Samahani sana, siwezi kuwauzia tena vifaa hivyo Bw. Mwichuli. Tayari mmeniingiza katika kashfa yenu bila ya kuniarifu. Na kamwe sitahusika tena katika kumsaidia huyo John Maina kuingia Ikulu. Tafuteni mtu mwengine!

**26. Mwichuli (via phone):** Pima maneno unayoyasema Alfayo Odhiambo! Unaweza kujikuta pabaya au kuangamiza biashara yako,...upo..? Pia tunaweza kuangamiza familia yako na kufanya maisha kuwa magumu sana kwako. Fikiria kwa makini jambo hilo.

**27. Alfayo:** **(angrily)** Sina haja ya kufkiria mara mbili, Mwichuli. Unaweza kuwasilisha ujumbe huu kwa mkubwa wako, kwamba nimekataa kula kwa kihorio kama yeye. Na zaidi nitahakikisha kuwa kashfa hii inafichuka hata kama ni kujitokeza hadharani. Siogopi tena!

**28. Mwichuli (via phone)** Ningekuwa wewe, ningefikiria kwa makini kauli hiyo. Na nakutahadharisha dhidi ya yote unayokusudia kufanya Alfayo. Bw. Maina si mtu wa kusahau haraka. Kamwe hawezi kusahau maneno haya. **(threatening)** Na endapo utajaribu kumporomosha basi hapana shaka wewe ndiye utakaye kuwa wa kwanza. **(phone goes dead)**

**28a. Alfayo:** **(to himself)** Balaa gani tena hili. Sasa nitafanyaje? Lazima nimweleze Jeffrey, kwani yeye anafahamu vizuri kashfa hii- lakini ataweza kunisaidia kweli..? Tayari ameachishwa kazi katika halmashauri ya kupambana na ufisadi?

**End of scene**

**29. Narrator:** Wapuliza kipenga ni watu wanaojitolea hadharani kutangaza maovu miongoni mwa jamii na kawe hawaogopi kusema kwa polisi au kwa umma. Ni watu wenye maadili bora na wasiopenda kuhusishwa na kashfa za aina yoyote au maovu katika jamii. Na hivi ndivyo anavyojihisi Alfayo. Yuko tayari kupinga kipenga kuhusu kashfa katika sekta ya niishati licha ya ukweli kwamba, anaweza kujikuta mashakani. Lakini wasi wasi wake mkubwa ni yale yatakayotokea baadaye!

## Scene Three:

**30. TV Anchor (on TV):** Karibu kwenye kipindi chetu cha mahojiano jioni ya leo. Katika studio tunaye mgeni mashuhuri John Maina ambaye pia ni miongoni mwa wanaogombea wadhifa wa urais kwenye uchaguzi mkuu ujao. Bw. Maina suala au hoja tunayoijadili hapa ni suala la ufisadi. Je, ni vipi utakabiliana nalo pindi utakapochaguliwa?

**31. Maina (in TV):** Bila shaka. Serikali yangu itapambana na uovu huu kuanzia mwanzo. Hatutakubali kamwe ufisadi kuanzia mashinani hadi ngazi za juu serikalini. Serikali yangu itakuwa na sera tofauti kabisa! Na hilo nakuhakikishia!

**32. SFX** **TV turned off**

**33. Alfayo:** **(shouting)** Huo ni upuuzi mtupu! Mwenyewe ametawaliwa na ufisadi. Tayari hisia zake zinachochewa na ufisadi hata kabla ya kuingia Ikulu...Je! Watu wanayaona haya yote? Anawezaje kuzungumza vile hadharani bila ya kuona haya?

**34. Isaac:** Baba punguza hasira! Hizi ni siasa. Wanasiasa wote wamepitia chuo kimoja cha kusema uongo. Na hata wewe mwenyewe unafahamu hilo! Wote ni sawa hakuna mkamilifu! Kuna watu wanaunga mkono kauli yake ile. Na watu anaowawakilisha watakuwa wakipanga foleni kupewa kitu kidogo baada ya kumchagua. Fikra zao ni kwamba endapo watamchangua basi watanufaika pakubwa. Hivyo ndivyo, siasa zinavyokwenda barani Afrika.

**35. Sylvia:** Mungu wangu, Isaac....inachukiza. Lakini usishangae amekuwa hivyo siku zote baba?

**36. Alfayo:** Sylvia, tofauti ni kwamba wakati tulipokuwa wadogo hatukuwa na vyombo vya habari vya kufichua kashfa za aina hii. Kwa hiyo ni tabia aliyokulia nayo tangu utotoni. Wengi hawafamu historia yake.

**37.Sylvia:** Ndio - lakini Baba...., licha ya ukweli kwamba tunawajua wahusika katika njama hii ya ufisadi, bado wako huru na wala hawajachukuliwa hatua zozote! Magazeti yamekuwa yakifichua au kuangazia uovu huu lakini wapi! Bado wahusika wako pale pale- Wanasiasa au wafanyabiashara mashuhuri. Hakuna mtu anathubutu kuwakamata au kuwachukulia hatua.

**38. Isaac:** Tunapaswa kuwa na mabadiliko, lakini nashangaa kwanini bado? Haya ndiyo, tunayojifunza katika Chuo cha Wanasheria: Kwamba hatimaye siku moja tutawakamata na kuweza kuwafungulia mashtaka. Hakika enzi inayokuja itakuwa ya kuwafagilia wote.

**39. Sylvia:** Au jamii zao zitawashinikiza kuwajibika kwao kama ilivyotokea kwa wale waliowatangulia. Huu ni kama mchezo wa kuuzunguka mbuyu si rahisi kumalizika.

**40. Jennifer:** Tosha sasa watoto mmeongea machungu yenu yote .Na hakika uovu huu unaweza kukomeshaw! Msingi ni kuwa na msimamo thabiti. Na nimekuwa nikisema haya mara kwa mara.

**End of scene**

**41. Narrator:** Sylvia ameuliza suala la msingi sana. Je! Inawezekana kukabiliana na ufisadi? Mambo yanaanza kuwa mabaya kwa familia ya Odhiambo. Wamekuwa wakimtazama Rais wao Mtarajiwa kwenye mahojiano kupitia Televisheni, akizungumzia suala la ufisadi na juhudi zake katika kuangamiza uovu huo, huku ikifahamika kwamba yeye ni fisadi nambari moja. Ni vipi hali hii itaweza kubadilika? Jennifer anaamini kuwa kinachohitajika ni watu wachache wenye ujasiri kuvunja mzunguko huu wa ufisadi.

**MUSIC (FADE UNDER OUTRO)**

**42. Narrator:** Hadi hapo tunafika mwisho wa makala haya ambayo ni sehemu ya nne katika mfululizo wa mchezo huu wa redio kuhusu ufisadi. Kwa jina "**Tembo Nyumbani**".

Katika kipindi kinachofuata tutasikia mipango ya Jeffrey katika kupambana na ufisadi, huku Isaac akishangaa baada ya kufahamu kwamba ufisadi umo ofisini mwake. Iwapo ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki tembelea mtandao wetu dw.de/lbe au pia ukiwa na maoni usisite kutututumia kupitia Facebook hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa!